

Tanroads: Hakuna barabara mwendokasi Kimara-Kibaha

Na Ikunda Erick

WAKALA ya Barabara Tanzania (TANROADS), Mkoa wa Dar es Salaam imesema hakuna barabara ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) iliyojengwa kuanzia Kimara mkoani Dar es Salaam hadi Kibaha mkoani Pwani.

Tanroads pia imesema barabara za njia nane zilizo-jengwa ziko wazi kwa matumizi ya magari ya kawaida.

Meneja mradi BRT Tanroads, Mkoa wa Dar es Salaam, Frank Mbillinyi alisema hayo alipozungunza na HabariLEO jana kuhusu kukamilika kwa upanuzi wa barabara za njia nane katika maeneo mengi kutoka Kimara hadi Kibaha.

Mbillinyi alisema serikali ilipanua barabara kutoka Kimara kwenda Kibaha ili magari yapite bila msongamano. Alieleza kwamba Tanroads walijenga njia nane kuanzia eneo hilo na wameshaondoa vizuizi, njia zikiwa wazi kwa magari kupita.

Alisema eneo wanaloweka vizuizi kwa sasa ni Kimara hadi Ubungo ambako upanuzi wa njia


nane unaendelea lengo ni kupunguza msongamano.

"Lakini tofauti na hapo, kwenye hizo njia nane kutoka Kimara kwenda Kibaha hakuna kizuizi kwa maana Tanroads hatujaweka kibao cha 'NO ENTRY' (hakuna kuingia), hivyo si kosa magari kupita na hakuna alama zozote za kalazo, njia iko wazi magari kupita," alisema Mbillinyi.

Kuhusu uwepo wa barabara za BRT katika barabara hiyo ya Kimara kwenda Kibaha, Mbillinyi alisema miundombinu ya mradi huo haijawahi kujengwa katika barabara hiyo kama ilivyodaiwa.

Mbillinyi alisema ujenzi wa barabara za BRT kutoka Kimara kwenda Kibaha uko kwenye awamu ya sita ya mradi wa miundombinu ya BRT itakayohusisha pia Barabara ya Mwai Kibaki-Kawe na Mbagala hadi Vikindu kama ilivyo kwenye mipango ya Wakala ya Mabasi Yaendayo Haraka (DART).

"Wenzetu wa DART wamepanga hivyo ila kwetu mradi wa BRT Kimara-Kibaha hatujaanza kuutekeleza kwa sababu bado haujafika



kwetu," alisema.

Aliongeza: "Hakuna vituo vya BRT katika barabara hiyo. Ujenzi wa barabara nane uliojengwa ni mradi tofauti kabisa, inawezekana wenzetu wa DART wana-peleka mabasi huku yale ya 'feeder' mwisho lakini kwenye mfumo wa ujenzi, sisi Tanroads hatujajenga njia ya BRT eneo hilo."

Mbillinyi alisema mradi wa BRT unatekelezwa kwa awamu sita na awamu ya kwanza ni ile ya kutoka Kimara kwenda katikati ya mji ambayo Tanroads wamejenga na kukamilisha tangu mwaka 2015 na tayari njia hizo zinatumika.

Awamu ya pili ya BRT ni kutoka Mbagala kwenda mjini na kuwa ujenzi wa miundombinu ya mradi huo ulikamilika tangu mwaka 2020 lakini watoa huduma za mabasi hayo walianza mwaka 2025.

Pia, awamu ya tatu ya ujenzi wa miundombinu ya BRT ni kutoka Gongolamboto kwenda mjini na kuwa mradi uko hatua za mwisho kukamilika. Vilevile, awamu ya nne ya BRT ni kutoka Barabara ya Sam Nujoma hadi Tegeta.

Mbillinyi alitafanua kuwa awamu ya tano ya ujenzi wa miundombinu ya BRT utatekelezwa kwenye Barabara ya Mandela na kwa sasa mchakato wa kumpata mkandarasi wa ujenzi unaendelea.

"Awamu ya sita ya BRT itahusisha Barabara ya Mwai Kibaki-Kawe, Kimara hadi Kibamba, Mbagala hadi Vikindu. Wenzetu wa DART wamepanga hivyo ila kwetu mradi hatujaanza kuutekeleza kwa sababu bado haujafika kwetu," alisema Mbillinyi.

Akizungumzia hilo, Meneja Tanroads Mkoa wa Dar es Salaam, Lazack Kyamba alisema tangu Novemba mwaka jana waliondoa vizuizi vyote katika Barabara ya Kimara-Kibaha ya njia nane na iko huru kwa matumizi, isipokuwa eneo la Kimara-Ubungo ambako ujenzi unaendelea.